MAUDHUI: RUSHWA YA NGONO

SIKU 16 ZA UANAHARAKATI

Utangulizi

Kwa mujibu wa kifungu cha 25 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na.11 ya Mwaka 2007; Rushwa ya ngono ni kitendo anachofanya mtu mwenye mamlaka, katika kutekeleza mamlaka yake kudai ngono au upendeleo wa aina yoyote kutoka kwa mtu kama kishawishi cha kumpatia huyo mtu ajira, cheo, haki, fursa au upendeleo mwingine.

Rushwa ya Ngono inapotolewa sehemu za kazi, au sehemu za kutolea huduma husababisha madhara mengi hasa kwa wanawake na wasichana. Baadhi ya madhara hayo ni kama kukwamisha upatikanaji wa haki, kusababisha mtendewa kukosa huduma muhimu za kijamii, kuongeza idadi ya wanawake na wasichana wenye maambukizi ya magonjwa ya zinaa kama UKIMWI nk. Vile vile Rushwa ya ngono inasababisha kudhoofisha nguvu kazi ya wanawake, wanawake na wasichana kutokua na kipato binafsi pamoja na kuzorotesha maendeleo na uchumi wa nchi kwa ujumla.

Maeneo hatarishi kwa rushwa ya ngono

Maeneo hatarish kwa rushwa ya ngono ni kama ifuatavyo;

Sehemu za Kazi: Mfano ya rushwa ya ngono kazini ni pamoja na waajiri kutoa ajira kwa wanawake na faida nyingine kama vile kupandishwa cheo, nyongeza ya mshahara, kupewa siku za kupumzika kwa kubalishana na kutoa ngono. Kutishia wanawake wengi kufanya ngono pia kwa kutishiwa na matokeo kama vile kupoteza kazi zao, ukosefu wa fursa za kupandishwa vyeo, kuongezwa mshahara nk. Utafiti uliofanywa na Chama cha Wanahabari Wanawake (TAMWA) nchini ulieleza kuwa wanawake asilimia 89% walioajiriwa katika sekta ya umma nchini wamewahi kuombwa rushwa ya ngono wakati wa kuajiriwa, kupandishwa vyeo au wakati wakihitaji huduma fulani (TAMWA, 2012).

Ofisi za Umma: Mfano ofisi zinazotoa huduma mbali mbali za usajili wa vyeti, utoaji wa leseni, vitambulisho, pasi za kusafiria nk, baadhi ya watumishi wanaweza kuomba rushwa ya ngono kwa kubadilishana na upatikanaji wa haraka wa nyaraka hizo.

Taasisi za Elimu. Taasisi za elimu kuanzia ngazi ya shule za msingi, sekondari na vyuo vikuu ni eneo hatarishi pia kutokea kwa rushwa ya ngono kwa walimu kuomba ngono kwa kubadilishana na alama za ufaulu nk. Kwa mfano; kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na taasisi ya kuzuwia na kupambana na rushwa nchini TAKUKURU, ukivihusisha vyuo vikuu vya Dar es Salaam na Dodoma, asilimia 50 ya waliohojiwa walieleza uwepo wa rushwa ya ngono katika vyuo vikuu, huku asilimia 29.9 ya wafanyakazi wakieleza kuwepo kwa ushawishi wa makusudi ili kujipatia huduma kutoka kwa mamlaka.

Maeneo mengine ya Huduma: Rushwa ya ngono inaweza kutokea katika meneo mengine ya utoaji huduma kama vile mahospitalini, mahakamani nk. Kwa mfano katika mahospitali kumekua na kesi kadhaa zikionesha madaktari wakishutumiwa kufanya ngono na wagonjwa ili kuharakisha matibabu yao, au kuwapatia dawa za matibabu.

Je Sheria Inasemaje Kuhusu Rushwa ya Ngono?

Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na.11 ya Mwaka 2007 imeweka kifungu mahususi cha kuzuia rushwa ya ngono ambacho kinabainisha kuwa mtu atakayefanya kosa hilo atakua amefanya kosa la rushwa na adhabu yake ni faini isiyozidi shilingi millioni tano (5), au kifungo kisichozidi miaka mitatu (3) au faini na kifungo kwa pamoja.

Serikali pia imeunda Kanuni za Mienendo na Maadili kwa Watumishi wa Umma chini ya Sheria ya Utumishi wa Umma zinakataza mtumishi yeyote wa umma kuwa na mahusiano ya kimapenzi na mtumishi mwenzake au mtu mwingine katika eneo la kazi na vitendo vyovyote vile vyenye kusababisha usumbufu wa kingono (Sexual harassment) mahala pa kazi. Aidha, kanuni zimekataza mtumishi yeyote kuweka sharti la ngono kwa mtumishi mwenzake; kubaka, kutomasa, kumshikashika mtumishi kwa makusudi kwa namna inayoashiria uhitaji wa ngono, kufanya au kuonesha ishara za vitendo, kelele na utani wenye kuashiria uhitaji wa ngono na kutoa maoni ya kingono dhidi ya mtumishi mwenzake.

Vyuo mbali mbali vimetengeneza Kanuni zinazoongoza watumishi wake, kwa mfano Kanuni za Maadili kwa Watumishi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Dodoma, zinakataza vitendo vya rushwa ya ngono au mahusiano ya kimapenzi kati ya mtumishi na mwanafunzi. Hali kadhalika zipo baadhi ya Taasisi na sekta binafsi zimepiga hatua kuwa na sera za kijinsia zinazokataza vitendo vya rushwa ya ngono pamoja na udhalilishaji wa kingono kwa ujumla wake.
Licha ya kuwa na Sheria na kanuni mbali mbali zinazokataza rushwa ya ngono bado vitendo hivi vinaendelea hasa katika sehemu za kazi, mashuleni na vyuo vikuu.

Je, kwanini vitendo vya rushwa ya ngono vinaendelea Kushamiri?

- Uelewa mdogo kwa jamii juu ya Sheria zinazozuia na kupambana na rushwa ya ngono, wala hawafahamu haki zao pale wanapoobwa rushwa ya ngono.
- Hofu kwa watendewa kuogopa kutoa taarifa kwa hofo ya kuachishwa kazi, kunyimwa huduma, kuachishwa masomo au kufelishwa kwa makusudi kwa wanafunzi hasa wa vyuo vikuu.
- Jamii inaendelea kupuuza na kutokuchukulia uzito suala la rushwa ya ngono
- Kosa la rushwa ya ngono ni gumu kuthibitisha kutokana na usiri
- Hivyo basi katika kipindi hiki cha Siku 16 za Uanaharakati, tunatumia kampeni hii kupaza sauti na kukemea vitendo vya rushwa ya ngono, lakini pia kutoa elimu juu ya Sheria na hatua zinazoweza kuchukuliwa ambapo mtu ataombwa rushwa ya ngono, au atanyimwa huduma kwa kukataa kutoa rushwa ya ngono.

Ungana nasi #Komeshaukatiliwakijinsiasasa #tokomezarushwayangono

Mtu Binafsi

Je umewahi kuombwa Rushwa ya Ngono? Je umewahi kushuhudia mtu akiombwa rushwa ya ngono? au unafahamu mtu anayefanyiwa unyanyasaji wowote kwa sababu ya kutakiwa atoe rushwa ya Ngono?

FUNGUKA! Usikae Kimya, hakikisha mtendewa anapata huduma na haki dhidi ya vitendo vya rushwa ya ngono, kwa kufanya yafuatayo;

Kataa Kutoa au Kupokea Rushwa ya Ngono: Pamoja na ukweli kwamba rushwa ya ngono ni kosa la kimaadili pia kosa la rushwa ya ngono ni kosa la jinai. Kwa hiyo mtu yoyote anapaswa kukataa kutoa au kupokea rushwa ya ngono. Kumbuka kwamba mtoaji na mpokeaji rushwa wote ni wakosaji.

Kemea Rushwa ya Ngono: Vitendo vya rushwa ya ngono ni ukatili wa kijinsia, uvunjifu wa haki za binadamu na huadhiri ustawi wa jamii. Utakaoshuhudia mtu akiomba au kuombwa rushwa ya ngono unapaswa kukemea na kuchukua hatua.

Toa Taarifa za Rushwa ya Ngono: Unapoona vitendo vya rushwa ya ngono vinataka kutendeka au vimetendeka toa taarifa kwa Mamlaka husika kama TAKUKURU. Kutoa taarifa za Rushwa ni wajibu wa kiSheria. Sheria mbali mbali kama vile Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Kifungu cha 39) kinatoa maelekezo jinsi ya kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kwenye mamlaka husika. Unaweza kutoa taarifa kupitia kupiga namba za msaada bure kwa mfano, kwa TAKUKURU kwa kupiga number **113** au kupitia mashirika yanayotoa msaada wa kiSheria kama vile Shirika la Wanawake Katika Sheria na Maendeleo Barani Africa (WiLDAF) **0800780070**, Kituo cha Sheria na Haki za binadamu (LHRC) **0800750035**, Chama cha WanaSheria Wanawake Tanzania (TAWLA) **0700751010**, Kituo cha Msaada wa KiSheria Kwa Wanawake (WLAC), **0800780100**.

Toa ushirikiano na Vyombo Husika Wakati wa Uchunguzi na Kutoa Ushahidi: Unapofanyiwa vitendo vya Rushwa ya ngono au kushuhudia vitendo hivyo shirikikiana na vyombo husika kutoa ushahidi ili Wahusika waadhibiwe kiSheria.

WiLDAF TANZANIA

MKUKI

Ungana nasi #Komeshaukatiliwakijinsiasasa #tokomezarushwayangono

Serikali

Je, kuna sera na Sheria madhubuti dhidi ya vitendo vya Rushwa ya Ngono? Je kuna mifumo wezeshi ya utoaji wa taarifa na msaada kwa watendewa wa vitendo vya Rushwa ya Ngono?

FUNGUKA! Boresha mazingira salama ya kisera na kiSheria katika kuzuia na kutokomeza rushwa ya Ngono, kwa kufanya yafuatayo;

Kuhakikisha mapitio na maboresho ya Sheria ili kuhakikisha upatikanaji wa haki kwa watendewa hasa kuongeza adhabu kwa wahalifu ziwe kali kama adhabu nyingine za matendo ya kingono kwa mujibu wa kifungu cha 130 cha kanuni za adhabu.

Kuhakikisha utekelezaji wa sera na Sheria ili kuleta mazingira salama mahali pakazi, sehemu za utoaji huduma pamoja na taasisi za elimu.

Kuimarisha mifumo ya Utoaji Taarifa: Uboreshaji wa mifumo ya udhibiti na uwajibikaji kwenye kuimarisha mifumo ya kusimamia maadili, mifumo ya utahini, mifumo ya kutoa taarifa na kulinda watoa taarifa pamoja na kuwajibisha watuhumiwa wa vitendo hivyo. Ikiwa ni pamoja na kutekeleza mpango wa uanzishwaji wa madawati ya jinsia kwenye vyuo vikuu ili kurahisishwa utoaji taarifa na huduma kwa watendewa wa matukio hayo.

Kuendelea Kujengea Jamii uwezo: Kendelea kuwajengea wanafunzi, wafanyakazi na jamii yote uelewa wa suala la rushwa ya ngono ili waweze kujitetea na kupambana nalo

Taasisi na Sekta Binafsi

Je taasisi yako ina sera dhidi ya unyanyasaji wa kingono? Je, taasisi yako inafumbia macho matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kingono? Je, taasisi yako ina mifumo ya kushughulikia masuala ya ukatili wa kijinsia hasa unyanyasaji wa kingono?

FUNGUKA! Zuia Rushwa ya Ngono katika Ngazi ya Taasisi kwa kuhakikisha yafuatayo;

Tengeneza na simamia utekelezwaji wa sera za jinsia hasa sera zinazozuia na kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kingono wa aina yoyote ile.

Tengeneza mifumo rafiki ya utolewaji wa taarifa na msaada kwa watendewa wa vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kingono katika taasisi, ikiwepo ulinzi wa ajira, masomo au haki stahiki ya mtoa taarifa.

Andaa mafunzo ya mara kwa mara kwa wafanyakazi juu ya ukatili na udhalilishaji wa kingono katika ulimwengu wa kazi.